

TAARIFA FUPI YA MRADI MDOGO (MICROPROJECT) CHINI YA UFADHILI WA SHIRIKA LA CHAKULA DUNIANI (FAO).

UTANGULIZI

Mkoa wa Kagera ulikumbwa na janga la Tetemeko la Ardhi mnamo **Septemba, 10 2016**. Tetemeko hili lilisababisha madhara makubwa kwa Mkoa wa Kagera na Taifa kwa ujumla. Mbali na Tetemeko la Ardhi Mkoa wa Kagera pia ulikumbwa na hali ya ukame na jua kali kwa kipindi kirefu. Hali hii pia ilitokea katika maeneo mengine ya Nchi yetu. Hali ya ukame wa muda mrefu ilisababisha mazao kukauka mashambani na mifugo kufa kwa kukosa malisho na maji; hali iliyopelekea kaya nyingi za Mkoa huu kuwa na upungufu wa chakula hivyo kuhitaji msaada wa chakula.

Baada ya hapo serikali na mashirika mbalimbali yalianzisha namna ya kukabiliana na majanga haya kwa sasa na kwa baadaye. **Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO)** likiwa mojawapo, limechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na majanga ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya katika Nyanja za Kilimo na usalama wa chakula kupitia wataalamu mbalimbali ambao wanaendelea kusambaza elimu hiyo kwenda kwa wakulima na wafugaji.

Ikiwa ni sehemu ya kukabiliana na majanga hayo, Shirika pia limefadhili fedha kuwezesha kutoa elimu kwa wakulima na wafugaji kupitia miradi midogo (**Microprojects**) kupitia vikundi vya wakulima na wafugaji.

Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa itapata jumla ya Shilingi **44,558,000** kwa ajili ya elimu na miradi hiyo midogo katika vikundi. Fedha hizi zitatolewa kwa awamu kila zinapotumika kwa kazi husika kwa mujibu wa Mkataba kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa na Shirika. Aidha fedha za mafunzo na uendeshaji tu ndiyo itatolewa kwa Wilaya, na manunuzi mengine yote yatafanywa na Shirika moja kwa moja.

Aidha Wilaya imeunda vikundi nane (8) vya Kilimo na Ufugaji ikiwa vitano (5) ni vya wafugaji na vitatu (3) vya wakulima Katika Kata za Songambe, Iteera, Kamuli, Mabira, Rukuraijo na Rutunguru. Vikundi vya kilimo vipo katika kata za Rukuraijo na Mabira na vya Ufugaji vipo katika kata za Songambe, Kamuli, Rutunguru na Iteera. Vikundi hivi vitajikita katika kilimo cha

migomba kwa kutumia mbegu zilizootehwa maabara (**Tissue culture**), kilimo cha mihogo (**Cassava cuttings**) na ufugaji wa kuku na nguruwe.

WAHUSIKA

Wahusika wakuu katika mradi huu ni vikundi vya wakulima na wafugaji, ikiwa ni **40%** wanawake, **40%** vijana na **20%** ni wa umri mchanganyiko. Mradi huu unatarajia kunufaisha zaidi ya Kaya zipatazo 240 kupitia vikundi hivi. Pia mradi huu utawezesha kutoa elimu kwa jamii nzima ya Wilaya ya kyerwa bila kujali uwepo wao kwenye vikundi vitakavyonufaika.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kupitia wataalam wake itajikita katika utoaji wa Elimu inayohusu kilimo kwa kuzingatia njia bora za kilimo na ufugaji wenye tija. Hii itafanyika kwa ushirikiano wa karibu na wataalamu kutoka kituo cha utafiti cha **Maruku kilichopo Bukoba – Kagera.**

MALENGO YA MRADI

Mradi huu ulianzishwa na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani kwa ajili ya kukabiliana na majanga mbalimbali kupitia elimu inayotolewa. Lakini pia kuweza kuinua kipato cha mwananchi katika kikundi, mtu mmojammoja na kaya. Aidha kupitia vikundi hivi inategemewa wananchi wasio katika vikundi watajifunza na kuiga mafanikio ya vikundi vya uzalishaji.

Aidha kufikia malengo na mafanikio tarajiwa Shirika linaomba ushirikiano mkubwa katika kusimamia na kuelimisha wengine kutoka kwa viongozi na wataalamu.

Wananchi wajitolee ili kufanikisha mradi huu kwa kuchangia nguvu na mahitaji mengine yaliyo ndani ya uwezo wao ili kufanya mradi uwe endelevu (Project sustainability).

Hali ya hewa ya Kyerwa ni nzuri kuweza kuzalisha mazao ya kila aina na ufugaji wa kisasa kwa mafanikio. Wakulima waelimishwe kujikita katika kilimo chenye tija na kibiashara zaidi kwa maendeleo yao.

KWA PAMOJA TUIJENGE KYERWA NA TAIFA LETU KWA UJUMLA